

Saba wafariki dunia kwa madai ya kula samaki wenye sumu

Na Julieth Mkireri, MAFIA

WATU saba wakazi wa vijiji vya Bweni na Kanga, Wilaya ya Mafia wanadaiwa kupoteza maisha baada ya kula nyama ya samaki aina ya kasa.

Tukio hilo linadaiwa kutokea Machi 12, majira ya saa mbili usiku baada ya kula nyama hiyo.

Akizungumza kwa njia ya simu, Mwenyekiti wa Kijiji cha Bweni, Juma Khatibu, alisema watu hao walikumbwa na umauti baada ya kuuziwa samaki huyo anayedaiwa kuwa na sumu.

Khatibu alisema samaki huyo haruhusiwi kisheria kuliwa na watu, lakini wapo wavuvi wanauziwa kwa njia za siri.

"Tukio hili lilitokea Machi 11, Jumamosi, hao wavuvi baada ya kuvua samaki huyo walimtingeneza kabisa wakiwa feru na wakawauzia wateja wao kwa njia ya siri, baada ya kula madhara yameanza kuonekana Machi 12 kwa wale wote walionunua," alisema.

Alisema kuwa kata zilizonunua samaki huyo wengine waliwagawia majirani ambao nao wameathirika.

Alisema hadi sasa vifo ni saba huku wagonjwa wanane wakielekea na matibabu katika hospitali ya wilaya na ya tarafa Kulongwe.

Hata hivyo inadaiwa wali-

ohusika kuuza samaki huyo hadi sasa hawajulikani walipo kwa kuwa baada ya kupata taarifa za madhara yaliyotokea hawa-jaonekana.

Mmoja wa waliokula samaki huyo, Shida Abdallah, mkazi wa Kijiji cha Bweni alisema wali-letewa na jirani yao ambaye alinunua kwa mvuvi.

Shida alisema wamekuwa wakila samaki huyo mara kwa mara, lakini kwa awamu hii ndio imewasababishia madhara.

"Jirani yetu kila akinunua kasa anatuletea tunakula, lakini hatupati madhara, safari hii tulipokula mimi niliumwa tumbo nikaenda kupata matibabu nimepona ila nimeshauriwa nisimnyonyeshe mtoto, yupo mmoja wa mama amefariki pamoja na mwanawe ambaye alikuwa bado ananyonya," alisema.

Diwani wa Kanga enco lilipotokea tukio hilo, Khatibu Faki, alithibitisha kuwapo na taarifa hizo na kwamba wananchi hao waliokufa kwa kula samaki aina ya kasa anayedhaniwa kuwa na sumu.

Kwa mujibu wa Diwani huyo kati ya vifo saba watoto ni sita.

Katibu Tawala Wilaya ya Mafia, Gilbert Sandagila, alikiri kuwapo kwa taarifa hizo ambaye alisema ukweli kuhusiana na chanzo cha tukio wanaendelea kufuatilia.

ma
cha
mi,
di,
ni
Ltd,
kesi
nba
wa
ad,
ara
25,
wa
wa
on-
la
4.4
ali

Serikali kujenga majosho nchi nzima

Na Lucy Ngowi

MTENDAJI Mkuu wa Wakala ya Masbura ya Veterinari Tanzania (TVLA) Dk Stella Bitanyi amesema Wizara ya Mifugo na

Uvuyi hivi sasa ina mkakati wa kuimarisha huduma za uogeshaji wa mifugo kwa kuwezesha halmashauri kujenga majosho nchi nzima.

Dk Bitanyi alisema hayo alipozungumza na HabariLEO kuhusu

wizara hiyo kupitia TVLA.

Alisema kila halmashauri ikiwa na majosho wakala utaendelea kuhakiki ubora wa hizo dawa za kuogeshea mifugo.

"Kwa hiyo sasa hivi mkakati wa wizara ni kuimarisha hizi

huduma za uogeshaji kupitia kuwezesha halmashauri kujenga majosho nchi nzima na kila kata ikiwezekana kupata majosho na sisi tunaendelea kuhakiki ubora wa hizo dawa," alisema.

Alisema kuna utaratibu wa

kuweka dawa kwenye majosho, ili kuendelea kudhibiti kupe lazima sampuli zichukuliwe zipimwe kupua kama uwezo umeshuka au la na kama ni wakati sahihi wa kuongeza dawa nyingine.

Kwa maelezo yake, dawa ikishaongezwa mara kadhaa, inabidi yale maji yote yatolewe na kuwekwa maji mapya na dawa mpya.